

Mei 21, 2015

Taarifa Kwa Vyombo Vya Habari

Matokeo Ya Hivi Karibuni Kutoka Mahakama ya Usuluhishi ya Kimataifa- ICC

Tarehe 13 Mei 2015, Jopo la Mahakama ya Kimataifa ya Biashara na Usuluhishi (ICC) katika kesi ya ICC Na. 20588 / ZF imetoa uamuzi wake kwa maombi ya Hatua za Muda iliyofunguliwa na AyoubFarid Michel Saab na Fadi Michel Saab, wadai katika mgogoro dhidi ya Jamhuri ya Cyprus.

Wakina Saab walileta maombi saba kwa hatua ya mpito katika maombi yao. Mahakama ya usuluhishi imeyaondoa madai sita kati ya hayo, kwa kuzingatia kuwa kuyaamua hayo kungeathiri uhalali wa kesi. Cha muhimu zaidi, uamuzi huu hauhusishi maamuzi ya mahakama hii kuhusu mwenendo wa Jamhuri ya Cyprus dhidi ya FBME Cyprus. Jopo la Mahakama litatathmini mwenendo wa Jamhuri ya Cyprus kwenye hatua ijayo, wakati itakapoamua juu ya uhalali wa mgogoro.

Cha muhimu, Jopo la mahakama limewapa akina Saab ushindi kwa ombi la mwisho.

Maamuzi ya jopo la usuluhishi la mahakama kuhusu ombi hili yanasomeka kama ifuatavyo:

[Dai Na. 7] limekubaliwa ambapo mshitakiwa (na vyombo vyake vya udhibiti) anatakiwa kujiepusha kuchukua hatua yoyote ambayo itaweza kuharibu kabisa biashara ya FBME Cyprus wakati tukisubiri kukamilika kwa kesi ya usuluhishi, na kuamriwa kutoa taarifa ya mwezi mmoja mapema kwenye jopo la mahakama ya usuluhishi, Wadai, Wakili wao, Bw Mafuru [Meneja Mdhibiti Maalum wa Benki Kuu ya Tanzania] na mamlaka nyingine zote husika na / au vyombo vyenye mamlaka hayo.

Hatua hii ni muhimu sana katika mgogoro huu kwa sababu mbili kuu:

- Kwanza, inathibitisha kiutaratibu Amri No 1 kwa kuikaribisha Jamhuri ya Cyprus ili kujiepusha kuendelea kuuza au kufanya utatuzi wa Benki ya FBME kabla ya mwisho wa usuluhishi huu.
- Pili, kwa kuweza kutoa taarifa kwa hatua yoyote kuhusu FBME Cyprus siku 30 kabla, Jamhuri ya Cyprus haiwezi tena kufanya maamuzi peke yake bila pande zote zinazohuzika kutaarifiwa kabla ya maamuzi kufanyika. Zaidi ya hayo, FBME, Jopo la Usuluhishi, Wakina Saab watakuwa katika nafasi ya kujipanga kabla ya uamuzi wa mwisho, na kuwa na nafasi ya kuchukua hatua zote za kisheria wanazodhani zinafaa.

Mwisho